Machoni mwa umma

Maoni ya wananchi juu ya upatikanaji wa taarifa



1. Utangulizi

Mwaka 1913, Jaji wa Kimarekani alisema “Mwanga wa jua ni kinga bora ya magonjwa”. Hakika, upatikanaji wa taarifa ni kama mwanga kwani unaweza kuzuia na kufichua rushwa na ubadhirifu. Hata hivyo, upatikanaji wa taarifa za Serikali ni zaidi ya uwazi wa vitendo vizuri au vibaya tu. Wananchi wanapofahamu msingi wa maamuzi serikalini, wanaweza kutathmini utendaji wa serikali na kuchangia mawazo yao. Je, kuna umuhimu wowote wa taarifa za serikali kutolewa kwa wananchi?

Tanzania ni miongoni mwa nchi za kwanza kujiunga na Mpango wa Uendeshaji wa Serikali kwa Uwazi(OGP). Mpango huu ni wa kimataifa wenye lengo la kuongeza uwazi wa masuala ya kiserikali kwa wananchi. Moja kati ya malengo ya OGP ni ushirikiano wa kuwajibika kwa pande mbili - yaani serikali na wananchi katika kuleta ufumbuzi wa changamoto zinazolikabili taifa. Hadi sasa, kama sehemu ya utekelezaji wa Mpango wake wa pili, serikali imedhamiria kutunga sheria ya uhuru wa upatikanaji taarifa itakayowarahisishia wananchi kupokea taarifa kutoka serikalini. Rais Kikwete alitoa ahadi hii kwenye kilele cha mkutano wa kimataifa mwezi Oktoba 2013. Muswada huo wa sheria ya habari uliwasilishwa Bungeni na kusomwa kwa mara ya kwanza mwezi Machi 2015.

Tanzania inaelekea katika uchaguzi mkuu miezi michache ijayo ya mwaka huu wa 2015. Katika muktadha huu, upatikanaji wa taarifa kwa wananchi unakuwa na umuhimu wa kipekee. Je, wananchi wataweza kupata taarifa wanazozihitaji ili kutathmini utendaji wa viongozi wao na kufanya maamuzi makini kuhusu maisha yao kupitia uchaguzi mkuu?

Muhtasari huu unawasilisha takwimu kutoka kwenye utafiti wa *Sauti za Wananchi*, wenye uwakilishi wa kitaifa unaofanyika mara kwa mara kwa njia ya simu za mkononi. Jumla ya wahojiwa 1,330 kutoka Tanzania Bara walipigiwa simu kati ya tarehe 23 Machi na tarehe 10 Aprili mwaka

Muhtasari huu umeandikwa na Youdi Schipper, Angela Ambroz, na Elvis Mushi
Muhtasari huu umeandaliwa na Twaweza East Africa.
Umetolewa Mei 2015

S.L.P. 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 266 4301
uwazi@twaweza.org www.twaweza.org/sauti

Twaweza ni sisi

2015. Hii ilikuwa ni awamu ya 31 ya utafiti wa *Sauti za Wananchi*. Kwa taarifa zaidi ya tafiti zilizopita (ikiwa ni pamoja na takwimu, dodoso, na mihtasari), tembelea www.twaweza.org/sauti

Dondoo za matokeo ya utafiti:

- Asilimia 84 ya wananchi wanaunga mkono kupitishwa kwa muswada wa sheria ya upatikanaji wa taarifa
- Asilimia 80 wanaunga mkono wananchi kupata taarifa, na kwamba upatikanaji huo utapunguza rushwa
- Asilimia 47 wanaunga mkono viongozi wa umma kuadhibiwa kwa kushindwa kuzingatia sheria
- Ni wananchi wachache tu huomba taarifa kutoka kwa watoa huduma. Na wanapofanya hivyo, hupewa taarifa hizo

2. Mambo sita kuhusu upatikanaji wa taarifa nchini Tanzania

Jambo la 1: Wananchi wengi wanaamini wanapaswa kupata taarifa za serikali

Asilimia 80 ya wananchi wanakubali kwamba upatikanaji wa taarifa unasaidia kukomesha rushwa. Wananchi wanapaswa kupata taarifa, na kwa wakati muafaka(Kielelezo cha 1), ingawa wananchi waligawanyika kuhusu iwapo taarifa za serikali zinaweza kufasiliwa kama "rasilimali za umma". Hata hivyo, bila kujali namna ambayo taarifa hutafsiriwa, wananchi waliowengi wanaamini kwamba kupata taarifa ni muhimu sana.

Maoni haya hayatofautiana sana kwa makundi mbalimbali. Tofauti pekee ilibainika kuwa: idadi kubwa zaidi ya wanaume inakubali kuwa "taarifa zinazozuiliwa na serikali ni rasilimali ya umma" kuliko ya wanawake, wakati waliohitimu darasa la 7 wana uwezekano mkubwa wa kukubaliana na kauli ya "wananchi wanapaswa kupata taarifa zinazozuiliwa na mamlaka za umma" (takwimu hazijaoneshwa).

Kielelezo cha 1: Kauli gani unakubaliana nayo zaidi?



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi* - Awamu ya 31 (Machi-Aprili 2015)

Jambo la 2: Wananchi wengi waliowahi kuomba taarifa serikalini walipewa

Ilibainika kuwa hata kama wananchi wengi walitembelea ofisi za serikali, wengi hawakuomba taarifa zozote kutoka katika ofisi hizi.

Hata hivyo, wananchi walipoomba taarifa walizozihitaji kutoka ofisi za serikali walipewa taarifa hizo (Kielelezo cha 2). Wananchi walitaja shirika la kusambaza maji kama ofisi iliyotoa majibu mengi zaidi ya maombi yote yaliyopokelewa kutoka kwa wananchi. Hata hivyo, hawakuulizwa ni taarifa gani zilizoombwa. Ofisi zilizosita zaidi kutoa taarifa zilikuwa ofisi za vyama vya siasa: waliopewa taarifa na vyama vya siasa hawakufika hata nusu ya wananchi walioomba taarifa hizo (ambao ni 13% kati ya 33%; Kielelezo cha 2).

Kielelezo cha 2: Je, ulipewa taarifa zozote ulizoomba ulipotembelea ofisi zifuatazo?



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi* - Awamu ya 31 (Machi-Aprili 2015)

Jambo la 3: Wananchi hawajui ni lini watapata taarifa walizoomba

Asilimia 12 ya wananchi wanaamini kwamba “hawatapa kabisa” taarifa walizoziomba kutoka ofisi za serikali (Kielelezo cha 3). Hata hivyo, idadi hiyo hiyo inadhani itapatiwa taarifa hizo mara moja. Idadi iliyobaki imegawanyika (Kielelezo cha 3). Pasipo sheria maalum inayosimamia maombi haya, uwezo ni mkubwa wa wananchi kutotambua watajibiwa lini.

Kielelezo cha 3: Iwapo ulituma maombi ya taarifa ofisi za serikali, unadhani ni muda gani utapita hadi upate jibu?



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi* - Awamu ya 31 (Machi-Aprili 2015)
Majibu ya "Sijui" na ambao hawakujibu, hayakujumuishwa.

Jambo la 4: Wananchi sita kati ya kumi wamesema wataripoti uhalifu kama wataona ukitendeka

Kufichua rushwa au vitendo viovu ni muhimu katika kujenga jamii huru na yenye haki. Hata hivyo, huwa ni kazi ya hatari kwa watoa taarifa za siri. Mara nyingi, wahalifu huwa na mtandao na nguvu kuliko ule wa wafichua siri.

Wananchi tisa kati ya kumi waliohojiwa walijibu kuwa kulikuwa na uwezekano mkubwa kwa wao kutoa taarifa kuhusu uhalifu (Kielelezo cha 4). Hata hivyo, hii inaweza kusababishwa na matamanio ya kila mtu kuamini kuwa anao uwezo wa kutoa taarifa za uhalifu.

Ni jambo la kuvutia kuwauliza wale wasemao hawana uwezo wa kuripoti uhalifu kwamba, ni kwa nini wana maoni hayo. Miongoni mwa waliosema hawataripoti uhalifu, mmoja kati ya wanne alidai kuwa ni hatari kufanya hivyo (takwimu hazijaoneshwa katika kielelezo, lakini idadi ni sawa na 4% ya watu wote).

Kielelezo cha 4: Wakati fulani wananchi huwa na taarifa kuhusu rushwa au uhalifu. Kama una taarifa kama hizo, je ungeweza kiziripoti?



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi* - Awamu ya 31 (Machi-Aprili 2015)

Jambo la 5: Wananchi wanataka viongozi waadhibiwe kwa kushindwa kutoa taarifa kama inavyoelekeza sheria

Tuliwapa wahojiwa orodha ya vipengele vitano vya muswada wa sheria ya upatikanaji wa taarifa, kisha tukawauliza ni kifungu gani muhimu zaidi kwao.

Kwa wananchi wengi, kipengele muhimu zaidi kilikuwa ni kile kilichowataka viongozi washitakiwe iwapo watashindwa kutimiza masharti yaliyoelekezwa na sheria – asilimia 47 walikiona kipengele hiki kama "muhimu zaidi" (Kielelezo cha 5). Hakuna kipengele kingine chochote kilichoungwa mkono kama hiki. Wananchi wana kiu ya kuona kuna uwajibikaji wa viongozi wa umma.

Kielelezo cha 5: Kipengele kipi katika muswada wa uhuru wa habari[1] kina umuhimu zaidi kwako?



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi* - Awamu ya 31 (Machi-Aprili 2015)

[1] Muswada wa sasa unaofanyiwa kazi na serikali unajulikana kama muswada wa sheria ya upatikanaji wa habari. Hata hivyo, wakati wa utafiti huu, tuliutaja kama muswada wa uhuru wa habari.

Jambo la 6: Muswada wa upatikanaji wa habari unaungwa mkono na wananchi walio wengi

Asilimia 84 ya wananchi wanauunga mkono muswada wa upatikanaji wa habari (kielelezo cha 6).

Kielelezo cha 6: Je, ungependa bunge lipitishe au lisipitishe muswada huu?



Chanzo cha takwimu: *Sauti za Wananchi* - Awamu ya 31 (Machi-Aprili 2015)

Tulipowaambia kuwa muswada utawataka viongozi wa umma kutoa taarifa za mara kwa mara kwa wananchi, njia iliyopendekezwa zaidi na wananchi wengi ilikuwa ni redio (takwimu hazijaoneshwa). Hususan, tulipowauliza - kwa ujumla – ni chombo gani cha habari wanachokiona kinaaminika zaidi, asilimia 60 walijibu kuwa ni redio (takwimu hazijaoneshwa).

3. Hitimisho

Sauti za Wananchi imegundua kuwa wananchi wengi wangependa kuimarishwa kwa uwajibikaji wa viongozi wa serikali na wanaunga mkono upatikanaji wa taarifa.

Takwimu hizi zinaonesha kuwa mitizamo ya wananchi kuhusu uwazi na uwajibikaji imejengwa na malalamiko yao ya muda mrefu kuhusu rushwa na sheria zisiyotekelezwa kwa ufanisi. Masuala ya kisera, kama vile kuwalinda watoa taarifa za siri, hayatajwi sana. Hiyo haina maana kuwa masuala hayo siyo muhimu.

Tanzania ni mwanachama wa Mpango wa Uendeshaji wa Serikali kwa Uwazi (OGP) na Mpango wa Uwazi Sekta ya Madini (EITI). Hivi karibuni, nchi yetu imepiga hatua kubwa katika programu ya takwimu wazi – yaani uanzishaji wa mfumo wa kitaifa kwa ajili ya kuziweka wazi kwa takwimu za serikali zinazohusu afya, elimu na maji. Takwimu kutoka *Sauti za Wananchi* zinaonesha kuwa maombi ya taarifa yanayotolewa na wananchi kwa ujumla hutimizwa na watoa huduma.

Hata hivyo, miswada miwili ya sheria iliyopitishwa na Bunge hivi karibuni- Sheria ya Takwimu na Sheria ya Makosa ya Mtandao – ina vipengele ambavyo vimeishia kuirudisha nyuma na hata kufuta hatua nzuri ambazo nchi yetu imepiga. Sheria ya Takwimu inatishia kutoa kifungo kikali na faini kwa mtu yeyote atakayechapisha taarifa za takwimu ambazo

ni “za uongo” au “zinapotosha”. Vile vile, Sheria ya Makosa ya Mtandao imeufanya uchapishaji wa “taarifa za kupotosha” mtandaoni pia kuwa ni kosa linalostahili adhabu ya kifungo au faini au vyote viwili kwa pamoja. Aidha, muswada wa upatikanaji wa taarifa na habari ulipelekwa bungeni kwa mara ya kwanza chini ya hati ya dharura iliyozuia fursa kwa wananchi kuuchunguza kwa undani zaidi. Kwa bahati nzuri, ratiba sasa imebadilishwa ili kuwapa wadau muda wa kuchangia maoni yao.

Ushahidi wa matokeo [2] haya na utafiti wa awali wa *Sauti za Wananchi* unaonesha kuwa wananchi wanaunga mkono dhahiri kabisa kuongezeka kwa uwajibikaji wa viongozi wa umma. Ingawa uhusiano wa dhana kati ya upatikanaji wa taarifa na uwajibikaji vinaweza kuwa siyo jambo la kutiliwa maanani sana na wananchi, takwimu hizi zinaonesha kuwa wananchi, kwa mapana, wnaunga mkono utoaji taarifa kwa umma kuingia kwenye sheria, na adhabu kali kuwekwa kwa watakaoshindwa kuzingatia sheria.

Msimamo wa serikali unaonekana kuwa na utata. Upo mvutano kati ya shauku ya kuiweka Tanzania karibu na kanuni za kimataifa za kuwa na uwazi zaidi, na utamaduni wa kihistoria wa “Siri kali” (usiri) wa kuficha taarifa hizi na kuendesha serikali wa usiri.

Serikali inashinikizwa na wananchi kuwa wazi zaidi. Pia imeweka agenda kabambe ya utawala wenye uwazi zaidi kupitia Mpango kazi wa Pili wa ushirikiano na serikali wazi. Lakini ahadi lazima ziambatane na vitendo. Serikali wazi ni lazima zifikie viwango vinavyotakiwa. Hii ni njia ya kuhakikisha serikali ipo kwenye upande sahihi kwa ajili ya wananchi wake na historia yake.

[2] *Sauti za Wananchi, Tanzania Kuelekea* 2015, Novemba 2014, Na. 18 na *Sauti za Wananchi, Kuwa na sheria, wakala na ahadi zaidi kunaleta mabadiliko?*, Na. 14, Agosti 2014

[h]ttp://www.opengovpartnership.org/sites/default/files/OGP%20ACTION%20PLAN%20PHASE%20TWO%2006.11.2014%20FINAL.doc